



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA



Toleo tarehe 21.10.2022

TAARIFA KWA UMMA

**MAAMUZI YA BARAZA JUU YA TUHUMA ZA UKIUKWAJI WA MAADILI YA
KITAALUMA ZILIZOKUWA ZIKIWAKABILI WAUGUZI NA WAKUNGA SITA.**

Baraza la Uuguzi na Ukunga ni Mamlaka ya Kisheria,inayosimamia Taaluma ya Uuguzi na Ukunga chini ya Sheria ya 2010,na kanuni zake za 2010,yaani **THE NURSING AND MIDWIFERY ACT 2010.**

Baraza la Uuguzi na Ukunga lilifanya kikao chake cha 212 tarehe 18 na 19 Oktoba 2022.Katika kikao hicho Baraza lisikiliza kikamilifu yaani (**Fully Inquiry**) Tuhuma mbili za ukiukwaji wa maadili zilizokuwa zikiwakabili Wauguzi na Wakunga sita,watano kutoka Hospitali ya Wilaya ya **Masasi-Mkomaindo**,na mmoja kutoka Hospitali ya OLTRUMET, wilaya ya Arusha DC.Baada ya kusikiliza Tuhuma hizo Wajumbe walifanya maamuzi yafuatayo:

NA	JINA	HOSPITALI/KITUO	ADHABU
1	Lucia Oswald Libaba (RN)	Hospitali ya Wilaya ya Masasi- Mkomaindo	Hakutiwa hatiani,aliachiwa huru
2	Elizabeth Rashid Njenga (RN)	Hospitali ya Wilaya ya Masasi- Mkomaindo	Alitiwa hatiani Amepewa KARIPIO KALI
3	Tumaini Hussein Millanzi	Hospitali ya Wilaya ya Masasi- Mkomaindo	Alitiwa hatiani Amepewa KARIPIO KALI
4	Joyce John Nkane	Hospitali ya Wilaya ya Masasi- Mkomaindo	Alitiwa hatiani Amefutwa kwenye Rejista ya wauguzi na Wakunga, amefutiwa leseni ya kutoa huduma za Uuguzi na


			Ukunga.
5	Pascal Aladin Mnyalu	Hospitali ya Wilaya ya Masasi- Mkomaindo	Alitiwa hatiani Amefutwa kwenye Rejista ya Uuguzi na Ukunga, amefutiwa leseni ya kutoa huduma za Uuguzi na Ukunga.
6	Rose Salvatory Saruma	Hospitali ya Wilaya OLTRUMET, Arusha DC	Alitiwa hatiani Amefutwa kwenye Rejista ya Uuguzi na Ukunga, amefutiwa leseni ya kutoa huduma za Uuguzi na Ukunga.

Adhabu hizi zimetolewa chini ya kifungu cha 28(3)(a)(c) cha Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya 2010. Aidha Wauguzi wengine watano, Mashauri yao bado yanafuatiliwa, yatasikilizwa katika kikao cha 213 cha Baraza. Wauguzi wote waliyotiwa hatiani, wana haki ya kukata Rufaa kwa Mh. Waziri wa Afya ndani ya siku 90.

Baraza linawakumbusha Wauguzi na Wakunga wote popote walipo, kuhakikisha wanatoa huduma kwa weledi na kufuata taratibu, Kanuni na Sheria. Kinyume cha hapo Baraza litaendelea kuchukua hatua kali za kinidhamu kwa watakao bainika kwenda kinyume na Maadili ya taaluma hii.

Aidha Baraza linapenda kuujulisha Umma kwamba adhabu hizi ni kwa Mujibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010 na kanuni zake, **na kwamba Sheria hii haina adhabu ya KULIPA FIDIA.**

Imetolewa na



Agnes Mtawa
Msajili,
Baraza la Uuguzi Na Ukunga Tanzania